



KISWAHILI

CORONAVIRUS NI NINI?

Ni kundi la virusi linaloweza kusababisha magonjwa kwa wanyama na binadamu. Kwa binadamu, kundi hilo la virusi linaweza kusababisha homa kali ya mapafu, na kusababisha matatizo ya Mfumo wa Upumuaji.

COVID-19 NI NINI?

COVID-19 ni maambukizi yanayotokana na badiliko jipya la virusi hivyo: ("CO" Corona, "VI" Virusi, "D" Maradhi na "19" mwaka ambao vilijulikana - 2019). Kabla ya kulipuka katika mji wa Wuhan huko China mwaka 2019, badiliko hili lilikuwa halijulikani.

DALILI ZA COVID-19 NI ZIPI?

Dalili za kawaida za ugonjwa huu ni homa, kikohozi kikavu, mwili kuchoka na kuumwa kichwa. Katika hali ya kuzidi inaweza kusababisha Homa kali ya mapafu, kubanwa mbavu na kupumua kwa shida (SARS) na hata kifo.

KUNA KINGA AU MATIBABU YOYOTE YA COVID-19?

Mpaka sasa ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja. Kinachofanyika ni kujaribu kutibu dalili mbalimbali za maambukizi hayo. Hivyo kama yalivyo magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo na ufuatiliaji wa karibu. Tafiti bado zinaendelea kutafuta kinga na matibabu yatakayo lenga maambukizi yenyewe.




NANI ALIYE HATARINI ZAIDI?

Ingawa tafiti bado zinaendelea kujua zaidi jinsi Covid-19 inavyoathiri, lakini mpaka sasa wenye hatari kubwa ni wale wenye umri mkubwa, waliodhoofika na magonjwa mengine (kama shinikizo la damu, moyo, saratani, kisukari) au wenye udhaifu wa kinga mwilini kutokana na sababu mbali mbali

NAWEZA VIPI KUJILINDA/KUJIKINGA NA KUPUNGUZA UENEZI WA MAAMBUKIZI?

Unashauriwa kufuata yafuatayo:

- Safisha mikono yako mara kwa mara kwa maji yanayotiririka na sabuni au kwa dawa ya kutakasa mikono (yenye alikoholi si chini ya asilimia 60) au angalau sekunde 20 kwa maji na sabuni.
- Epuka kuingia katika msongamano mkubwa wa watu maana wenye virusi hawaonekani kirahisi. Kaa mbali angalau mita 1 au 2 na mtu mwenye dalili za homa au kikohozi mwenye historia ya kusafiri maeneo yenye mlipuko wa ugonjwa huo.
- Epuka kugusa macho, pua na midomo kwa mikono. Mikono inagusa vitu vingi na inaweza kuchukua virusi. Virusi vikiwa katika mikono, vinaweza kuhamia machoni, puani na mdomoni. Kutoka hapo, vinaweza kuingia mwilini na kukuathiri.
- Hakikisha wewe na walio karibu yako mnajikinga kwa kuzingatia taratibu za usafi za mfumo wa kupumua. Hii inamaanisha tumia karatasi za shashi (kama huna, hata karatasi ya choo / toilet paper) uitumie kuziba pua na mdomo ukikohoa au kupiga chafya, halafu uitupe mahali pa takataka. Kama hauna tumia pindi ya mkono wako (kiwiko cha mkono wako) kuinga wakati wa kupiga chafya au kikohozi.
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana au kubusiana. Bakia nyumbani kadri inavyowezekana, kama ulivyoelezwa na mamlaka husika. Ukiwa na homa, kikohozi, au kupumua kwa shida wahi kituo cha huduma za afya au tafuta ushauri wa matatibu – lakini piga simu kabla ya kwenda ili ushauriwe vizuri sehemu ya kwenda. Hii itasaidia pia kukulinda na kuzuia uenezi wa maambukizi haya na mengine. Subiri au epuka safari zisizo za lazima kwenda kwenye maeneo yaliyoathirika.



All the measures included in the present leaflet follow what established by the world health organization (WHO)